TANGAZO LA SERIKALI NA. 265 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MISITU NA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanya ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Tafasiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktradha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi; mimea, hewa,viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji unaozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hii au sheria nyingine

yoyote;

"kiwanda" maana yake ni jengo au majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa misitu au visiki;

"maeneo ya malisho" maana yake ni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri kwa ajili ya malisho;

Sura ya 191 "maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 323 "mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu;

Sura ya 191 "mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa Shinyanga au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

Sura ya 323 "misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

Sura ya 191 "taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 "taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"uchafu wa mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

"udongo" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu ufuatao:
(a) kuingia na kukagua nyumba, kiwanja, barabara, njia, uchochoro, mfereji au ardhi na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu au laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake; na
(c) kutoa miongozo, kanuni na taratibu za kiafya kwa ajili ya wananchi wote kuzifuata.

Taratibu za kilimo

Sura ya 113

5.-(1) Mtu anayekusudia kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria za Ardhi na sheria nyingine.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika shamba lolote kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa dhumuni la kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Katazo

6.-(1) Mtu hataruhusiwa kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito au mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira.

(2) Mtu hataruhusiwa kutumia ardhi kinyume na matumizi ya kilimo kama yalivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Mtu hataruhusiwa kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya kanuni ndogo ya (3) kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(6) Mtu hataruhusiwa kumiliki eneo la chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(7) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa mabaki ya vifungashio vya viuatilifu au kusafisha vipulizi au

kumwaga mabaki ya viuatilifu katika chanzo cha maji au mto.

Uhifadhi wa uoto wa asili

7. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanapanda miti ili kutoendelea kuharibu mazingira na kurejesha uoto katika hali yake ya asili.

Uchimbaji mchanga na kokoto

8.-(1) Mtu hataruhusiwa kuchimba mchanga au kifusi au kuchoma tofali katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa, kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

(2) Mtu hataruhusiwa kujenga nyumba au jengo lolote au kufanya shughuli zozote za kiuchumi katika eneo la hifadhi.

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

9.-(1) Halmashauri ina wajibu wa kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji na mazingira bila sababu ya msingi.

(3) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa inazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

(4) Halmashauri na jamii husika ina wajibu wa kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(5) Mtu hataruhusiwa kulima, kukata miti au kuchunga mifugo katika umbali wa mita sitini kutoka chanzo cha maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

Uchafuzi wa

10.-(1) Mtu hataruhusiwa kuelekeza mabomba ya

vyanzo vya maji

maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe hai wengine.

(2) Mtu hataruhusiwa kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe hai chochote.

Kuchoma au kusababisha moto

11.-(1) Mtu hataruhusiwa kuchoma au kusababisha moto katika misitu katika eneo la Halmashauri.

(2) Itakuwa ni wajibu kwa kila mkazi kuzima moto ambao utaonekana kuwaka katika eneo la Halmashauri wenye kuleta viashiria vya hatari au kuharibu misitu.

Kibali cha kuchoma moto

12.-(1) Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza atalazimika kutoa taarifa ya siku mbili kabla ya kuchoma moto kwa majirani katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto kusambaa katika maeneo mengine.

(2) Muda unaoruhusiwa kwa mtu kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa nne kamili asubuhi.

Uvunaji wa miti

13.-(1) Mtu anayetaka kuvuna mti au miti kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote ni atapaswa kupata kibali cha Halmashauri kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna mti au miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe hai maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(3) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa wanatakiwa kuwa na eneo maalumu lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa na kufuata taratibu zilizowekwa na Halmashauri.

Wajibu wa

14. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika-

kupanda miti

(a) kupanda na kutunza miti katika eneo na makazi yake; na
(b) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

Wajibu wa Kata

15. Kata itawajibika kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Wajibu wa Mtaa

16. Kila Mtaa utahakikisha -
(a) unatunza miti yote inayopandwa katika eneo la Mtaa;
(b) unasimamia kila kaya kupanda miti na kuwa na miti isiyopungua kumi katika eneo la nyumba yake;
(c) unasimamia kila shule au taasisi nyingine ndani ya Mtaa inapanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake;
(d) unatunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;
(e) kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto bila kibali na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake;
(f) unahamasisha wakazi wa mtaa husika kuwa na msitu wa hifadhi ya miti ya kupandwa au ya asili kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi na mazingira; na
(g) kila mtu mwenye nyumba au kiwanja anawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba au kiwanja chake na kuitunza.

Utupaji wa taka ngumu na laini

17.-(1) Mtu yeyote anatakiwa kutupa taka katika eneo maalumu lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kutupa taka ngumu au laini.

(2) Mtu hataruhusiwa kutupa taka ngumu au laini,

kujisaidia katika kingo za mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri.

Uendeshaji wa viwanda, vituo vya mafuta, huduma za ujenzi

18.-(1) Mtu anayeendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe hai wengine katika maeneo ya makazi ya watu atatakiwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii.

(2) Endapo mtu yeyote anataka kuendesha shughuli za kiwanda, kituo cha mafuta au kituo cha huduma mbalimbali za ujenzi atatakiwa kuzingatia tahadhari za athari za mazingira.

Makosa yanayohusu mazingira

19. Mtu anatenda kosa endapo:

(a) ataingiza mfugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(b) atasafirisha mfugo bila kuwa na kibali;
(c) atalisha mfugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;
(d) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo;
(e) atakiuka masharti ya kilimo;
(f) atakiuka masharti ya kuhifadhi ardhi;
(g) ataharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;
(h) atabainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe hai wengine;
(i) atatupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa; au
(j) atatiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

Makosa yanayohusu

20. Mtu anatenda kosa endapo:

(a) atachoma au kusababisha moto katika misitu

kuvuna, kuuza, kusafirisha na kuhifadhi mazao ya misitu

bila kibali;

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi;

(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali;

(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali;

(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;

(f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti, eneo lililohifadhiwa kama bustani ya miti, misitu ya asili au iliyopandwa kwa ajili ya hifadhi;

(g) atakata miti au kuchunga mifugo kwenye eneo lenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kukinga upepo;

(h) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila kuwa na kibali; au

(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Adhabu

21. Mtu atakayepatikana na hatia kwa kosa lililotendwa kinyume na Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote.

Kufifilisha kosa

22. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(4) na 12)*

KIBALI CHA KUCHOMA MOTO

1. Jina la Mwombaji…….……………………………..............................

2. Simu Na………………anapoishi (kijiji au mtaa) ………………………………
katika Kata ya ………………Wilaya ……………………….

3. Lilipo eneo analotaka kuchoma moto (kijiji au mtaa) ………………………Kata ya……………….
Sababu ya kuchoma moto…………………………………………………….

4. Aina ya eneo analotaka kuchoma moto ………………………………na idadi………………………Ukubwa (DBH)…………………………………….

5. Malipo ya kibali (Shilingi)………………Namba ya stakabadhi…………………….

6. Jina la Afisa aliyefanya ukaguzi………………………………………

7. Wadhifa………………………………. Saini…………………….

8 Tarehe………………………

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 13)*

KIBALI CHA KUVUNA MTI AU MITI

1 Jina la Mwombaji………. …………………………………….........

2 Simu Na……..................…anayeishi (kijiji au mtaa)……….......
katika Kata ya …………Wilaya …………………………

3. Eneo mti au miti ilipo (kijiji au mtaa) …………………………Kata ya………………………
Sababu ya kuvuna………………….........…………………………………

4. Aina ya mti au miti ……………………………………………………na idadi…………………………………Ukubwa (DBH)………………..

5. Malipo ya ushuru (Shilingi)…………………Namba ya stakabadhi……………………..

6. Jina la Afisa aliyefanya ukaguzi………………………………………………

7. Wadhifa……………………………. Saini………………………………….

8 Tarehe………………………

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Misitu na Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi ................

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina: …………………………………..……………………
Saini………………………..……………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe………………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano uliofanyika Tarehe 23-24/3/2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya;

MWL ALEXIUS REVOCATUS KAGUNZE
*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga*

MH. ELIAS RAMADHANI MASUMBUKO
*Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga*

L.S

NAKUBALI

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*